SautiElimu

Toleo la 13
2006
ISSN 1821 5076

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Elimu kwa wote: mtoto wa kike alindwe

Na Newton Kyando, HakiElimu

Harakati za kuboresha elimu zimeleta matunda bayana. Watoto wengi wanaandikishwa kujiunga na shule zetu, waalimu zaidi wanaajiriwa, madarasa zaidi yanajengwa pamoja na mambo kadha wa kadha. Sote tumeyaona na tumeyakubali. Kuna jambo moja muhimu ambalo linapaswa kupewa uzito sambamba na mafanikio haya. Nalo ni ulinzi wa ziada na mwamko wa kipekee unaolenga kuhakikisha kuwa wasichana wanapewa nafasi sio tu ya kuandikishwa shule bali pia kuendelea na masomo hadi kuhitimu.

Tunapaswa kufanya hili, kwa kuzingatia mapungufu kadhaa yaliyojitokeza dhidi ya mafanikio ya elimu. Sehemu kubwa ya watoto wanaoandikishwa shule hawafanikiwi kuendelea na masomo hadi kuhitimu. Wengi wa watoto hawa wasiomaliza shule ni wasichana, tena kutoka familia za watu masikini. Tafiti zimebaini kuwa kuna mambo mengi yanayochangia watoto wetu kushindwa kumaliza masomo. Mambo hayo ni pamoja na:

Unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia unaofanywa katika jamii zetu ama mashuleni; Kazi wanazopewa watoto majumbani ambazo zinauzidi uwezo wao kiumri; Watoto kuozeshwa wakiwa masomoni; Familia kushindwa kuhimili gharama za maisha; Watoto wa kike kupewa nafasi finyu katika elimu, kupata ujauzito wakiwa masomoni na matatizo mengine kadha kama hayo.

Ikumbukwe kuwa matatizo haya hayawakumbi wasichana pekee. Lakini ni ukweli usiopingika kuwa sehemu kubwa ya waathirika ni wasichana na mbaya zaidi kuna matatizo mengine ambayo huwapata wao peke yao.

Kwa vile watoto hawa ni sehemu ya jamii yetu, basi ni wajibu wetu sote kuwalinda. Jamii inapaswa kuwalinda wasichana hasa ikizingatiwa kuwa wafanyiwayo wasichana hawa tunayaona. Kila mtu achukue wajibu kuijulisha serikali juu ya vikwazo hivi pamoja na vingine vyote vinavyokwamisha elimu. Wasichana hawa ni mama wa kizazi kijacho, kuwanyima elimu kwa sababu yoyote ile ni kuangamiza kizazi kijacho!

Kumzuia mtoto aliyepata mimba kupata elimu ni ukiukwaji wa haki za binadamu

Na Godfrey Telli, HakiElimu

Mtoto aliyepata mimba ni mtoto pia. Kimantiki anapaswa kupatiwa haki zote wapatazo watoto wote ikiwemo elimu. Tafiti mbalimbali zinaonyesha kwamba watoto wa shule hawapati mimba kwa kudhamiria. Ni wahanga wa udanganyifu na ushawishi kutoka kwa watu wazima.



Zoezi la kuwafukuza shule watoto wa kike waliopata mimba ni ukiukwaji wa haki ya msingi ya mtoto wa kike kupata elimu. Si tu kwamba zoezi hili linamuondoa mtoto huyu katika mchakato wa kupata elimu, bali pia linamuondolea matumaini yake ya maisha na maendeleo kwa siku za baadae. Kwa mtoto wa kike fursa za kujipatia maendeleo yake ya baadae ni finyu ikilinganishwa na mtoto wa kiume. Elimu ni njia pekee kwake kujipatia maendeleo. Kwa hiyo kumzuia kupata elimu ni kumzuia kupata fursa nyinginezo kama vile kupata ajira, chakula bora, malazi, matibabu, nk.

Kupata mimba kunachukuliwa kama ni uvunjaji wa baadhi ya sheria za shule. Hata hivyo kufanya makosa ni sehemu mojawapo ya tabia ya asili ya mtoto. Na kwa kuwa ni kawaida kwa kila kosa kuadhibiwa, si sahihi kumnyima mtu haki yake ya msingi ya kibinadamu kama adhabu kwa kosa alilotenda. Kama ni lazima, basi njia nyingine za kinidhamu zitumike.

Kupata mimba kunahusisha watu wawili. Lakini kwa jinsi hali ilivyo ni mtu mmoja tu anayeadhibiwa. Kwa kawaida aliyempa mimba msichana huwa hakuna juhudi za dhati zinazochukuliwa kumshughulikia.

Katika jamii zetu mtoto wa kike akipata mimba huonekana kama 'ameifedhehesha jamii nzima kwa kufanya matendo ya aibu'. Lakini cha kujiuliza hapa ni kwamba hivi ni wasichana tu wenye jukumu la kulinda maadili mema ya jamii? Wako wapi wanaume ambao ni chimbuko la hili tatizo la mimba? Kwa hiyo basi, zoezi hili sio tu ni kuzuia haki ya msichana kupata elimu, bali pia ni ubaguzi wa kijinsia dhidi ya mtoto wa kike.

Tuwajibike sote kwa pamoja kutatua tatizo hili la mimba miongoni mwa wanafunzi. Tusiwaachie watoto wa kike kutoka familia masikini kubeba jukumu hili peke yao wakati ni tatizo la jamii nzima. Tuzingatie haki za binadamu, hususan haki ya mtoto kupata elimu. Tunapaswa kuhakikisha kila mtoto anapata haki yake bila kisingizio chochote kile.

Watoto wote wana haki ya kupata elimu. mtoto aliyepata mimba ni mtoto pia!

Msichana asiwekewe vikwazo kupata elimu

Na Prisca Pius, Mwanza

Kwanza napenda kutoa shukurani zangu kwa Marafiki wenzangu wa elimu. Jambo muhimu ninalotaka kuwajulisha ni umuhimu wa kuwapatia watoto wa kike elimu bora. Tunafahamu Serikali imejitahidi kufanya hivyo lakini bado juhudi zaidi zinahitajika.

Hebu fikiria mtoto wa kike amesoma kwa takribani miaka 11, yaani darasa la kwanza hadi kidato cha nne, kwa kusumbuka na kujitahidi sana. Halafu inatokea kwa bahati mbaya anapata mimba dakika za majeruhi; anapokaribia kufanya mtihani wake wa kidato cha nne. Kweli hapo kuna sababu gani ya kumfukuza shule? Ni kwa faida ya nani? Kwa nini wasimuache afanye mitihani yake ya mwisho?

Kitu kibaya zaidi ni kwamba utakuta mtoto mwenyewe anajiweza sana kimasomo. Na akifanya mitihani ataweza kufikia malengo yake ya maisha. Lakini walimu watafanya kila liwezekanalo ili kuhakikisha hafanyi mitihani yake na anafukuzwa shule.

Ninaiomba Serikali iliangalie upya suala hili ili watoto wa kike wanaopata mimba wakiwa shuleni waandaliwe utaratibu wa kuweza kuendelea na masomo yao hadi mwisho wa kikomo cha uwezo wao. Wote tunafahamu kiungo kikubwa cha jamii yetu ni mwanamke, lakini wao ndio wenye matatizo sana wakiwa shuleni. Tatizo lipo kila mkoa lakini hapa kwetu Mwanza nadhani limezidi zaidi na linawaumiza wasichana wengi.

Pia suala la kuwanyanyapaa wasichana naomba liangaliwe kwa mapana zaidi. Wapo watu wanaoamini kwamba mtoto wa kike hawezi kuwazidi wavulana darasani. Msichana akiongoza wanasema ametoa rushwa ya ngono; 'eti amepewa maksi za chupi' Hii yote sababu yake ni kwamba wanaamini mtoto wa kike hawezi kufanya vizuri darasani. Huu ni unyanyapaa ambao ninaomba ukomeshwe.

Sheria inamkandamiza mtoto wa kike

Na Veronique Kilala, Sumbawanga, Rukwa

Salamu kutoka kwangu rafiki yenu. Ninapenda kutoa mchango wangu kupitia jarida la *SautiElimu ili* uwafikia watu wengi katika jamii yetu.

Mchango wangu unahusu sheria inayotoa kibali kwa mtoto kuolewa akiwa chini ya umri wa miaka 18. Mimi nadhani sheria hii inapaswa kufikiriwa zaidi na kufanyiwa kazi upya. Ukweli ni kwamba sheria hii inambana na kumkosea haki ya masomo mtoto wa kike.

Ni ukweli usiopingika kwamba kama mtoto wa kike akianza shule akiwa na umri wa miaka 7 kulingana na sheria hii itakuwa vigumu kwake kuendelea na masomo hadi kuvuka kidato cha nne. Sheria hii inamuandaa kuolewa na wala sio kusoma hadi ngazi ya juu.

Mimi ninaamini kwamba elimu ni haki yetu sote; watoto wa kiume na wa kike. Sheria hii haimpi mtoto wa kike fursa sawa na mtoto wa kiume katika kujiendeleza kielimu. Kumbe ndio sababu sisi watoto wa kike tuko nyuma kielimu na kimaendeleo!

Baadhi ya wazazi wanatumia mwanya wa sheria hii kuwaozesha watoto wao wa kike wakiwa bado katika umri mdogo na kuwakatiza masomo yao. Hivyo Serikali inatakiwa kuiangalia kati sheria hii na kuitazama kwa undani zaidi.

Ninawaomba viongozi wanawake walioko serikalini na bungeni kutoa msukumo ili sheria hii ifutwe kwa lengo la kutusaidia sisi wasichana kupata elimu na maendeleo. Na kwa kuwa kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete ni "Maisha Bora kwa kila Mtanzania" tunamuomba atusaidie sisi wasichana kupata elimu na hatimaye nasi tuwe na maisha bora kama wanaume.

SautiElimu

Toleo la 13
2006
ISSN 1821 5076

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Barua kwa SautiElimu

Elimu kwa msichana vipi?

Na Wilbard Nyakwana, Dar es Salaam

Pamoja na kuwepo na maendeleo katika sekta ya elimu hapa nchini kupitia programu za MMEM na MMES bado kuna vikwazo lukuki katika kuwapatia elimu watoto wa kike. Baadhi ya vikwazo hivi ni pamoja na:

- Kukosa wazazi na wao kuchukua jukumu la kutunza familia
- Kazi nyingi za nyumbani
- Kupata mimba zisizotarajiwa
- Kunyanyapaliwa

Sababu nyingine zinazofanya elimu kwa mtoto wa kike kuwa ni suala la kubahatisha tu ni mila na desturi mbaya zinazomkandamiza mtoto wa kike. Pia mazingira duni sana ya familia nyingi yanamuumiza zaidi mtoto wa kike na kumfanya ashindwe kuendelea na masomo yake.

Ili kuboresha elimu ya msichana mambo yafuatayo yazingatiwe:

- Utaratibu wa kufundisha na kujifunza uwe shirikishi unaomthamini mtoto wa kike
- Mazingira ya shule yaboreshwe kumlinda mtoto wa kike
- Uhusiano kati ya walimu na wanafunzi uwe bora, wa kuaminiana na wa kimaadili

Mwisho natoa wito kwamba mtoto wa kike aandikishwe na kubaki shuleni hadi kuhitimu. Apate elimu itakayomsaidia maishani. Elimu kwa mtoto wa kike itasaidia kuboresha familia nzima yaani baba, mama na watoto watakaowazaa.

Wasichana wapatao mimba waendelee na masomo

Na Mercy Masasi, Dar es Salaam

Mercy Masasi ni Rafiki wa Elimu anayeguswa sana na tatizo la watoto wa kike wanaopata ujauzito wakiwa shuleni, ambao wanakosa haki ya kupata elimu ya kuwasaidia kumudu maisha yao.

Anasema kwamba suala la elimu bado ni muhimu mno. 'Kuna dhana potofu katika jamii ambayo

watu wanachukulia kwamba mtoto wa kike akishapata ujauzito hana tena haki ya kuendelea na masomo. Mimi nadhani jamii iangalie ni vitu gani vinavyomfanya mtoto wa kike kupata ujauzito, maana kuna mambo mengi' Mercy anasema.

Anaongeza kuwa kutokana na uzoefu wake, tangu alipokuwa anasoma shule ya msingi, kuna mambo mengi anayojua yanayosababisha watoto kupata ujauzito. Anasema chakula na malazi vinasababisha baadhi kushindwa kuendelea na shule, kwa kuwa wengi hupelekwa shuleni bila kupata mahitaji hayo. Hata hivyo wengi zaidi hufukuzwa kwa kupata ujauzito kwa kudanganywa kiurahisi kwa sababu ya ukosefu wa elimu ya uzazi na matatizo yaliyotajwa.

Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba watoto hao wanapokosa elimu baadae wanakuwa tegemezi kwa jamii. Watoto waliozaliwa wanabaki katika hali duni ya malezi na hali ya jamii kwa ujumla hubaki kuwa duni tofauti na kama mtoto huyu angeruhusiwa kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

Mercy anasema si lengo lake kuchochea vitendo vya ufuska na kusababisha mimba zisizotarajiwa shuleni kwa kuwatetea watoto hawa wanaopata mimba shuleni. Bali ni kutaka waendelee kupata elimu itakayowakwamua kimaisha.

Anamalizia kwa kuitaka Serikali iwape wasichana nafasi ya kuendelea na masomo yao baada ya kupata mimba bila masharti yoyote.

Mazinduke na wasichana Ukerewe

Na Sospeter M. Julius, Ukerewe

Mazinduke ni muziki wa usiku ama disko ambalo kwa kawaida huvutia watu wengi wakiwepo wanafunzi. Mazinduke yamekuwa ni chanzo cha kushuka kwa kiwango cha elimu wilayani Ukerewe. Wanafunzi wa kike ndio wanaoathirika zaidi.

Si ajabu kukuta wanafunzi wengi hapa Ukerewe hawajui kusoma wala kuandika. Lakini Mazinduke wanayajua kupita kiasi. Ukimwita msichana yoyote wa shule ya msingi na kumuuliza 1 x 3 usishangae akikuambia ni 13. Lakini mtoto huyo huyo ukimwambia akuimbie wimbo wa msanii Bushoke atakuimbia wote hadi mwisho bila kukosea.

Ninawaomba Marafiki wa Elimu kwa kushirikiana na wadau wengine wote wa elimu wafuatilie suala hili ili kupata watoto walioelimika vizuri, watakaolisaidia taifa. Bila kuingilia kati suala hili mapema Ukerewe itaangamia na taifa zima pia litaangamia. Elimu ni muhimu sana hususan kwa siku zijazo.

Mambo yanayochangia kushuka kwa elimu yetu

Na Lulenga C. Tilwebwa, Nansio - Ukerewe

Napenda kutoa maoni yangu kuhusu mambo yanayochangia kuwepo kwa matokeo mabaya katika shule zetu.

Jambo la kwanza ambalo kwangu mimi naliona ni baya sana ni kwa walimu kuamua kufanya mapenzi na wanafunzi wao wa kike. Na mara nyingi hali hii hujitokeza zaidi kupitia zoezi la 'tuisheni'. Tuisheni hizi mara kadhaa malengo yake yanakuwa si mema. Zinatumiwa vibaya na baadhi ya walimu ili kuwanasa watoto wa kike.

Ninawaomba walimu na wazazi kwa kushirikiana na Kamati za Shule kuzifanyia tathmini tuisheni zote na pale inapobainika kwamba zina malengo mabaya basi zidhibitiwe na wahusika washughulikiwe mara moja.

Jambo lingine linalosababisha matokeo mabaya shuleni ni pale wazazi wanapodiriki kutoa rushwa kwa walimu kwa lengo la kuwasaidia watoto wao kufaulu mitihani yao ya kitaifa. Hii si tabia nzuri, kwani inashusha kiwango cha elimu yetu kwa kuwabeba watoto wasio na uwezo darasani na kuwatelekeza wale wenye uwezo zaidi.

Pata machapisho mapya kutoka HakiElimu!

HakiElimu ni shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora, haki na demokrasia katika elimu na jamii. Tunafanya hivyo kwa kuwezesha jamii kupata habari, kubadili shule na mfumo wa uundaji wa sera; kuchochea ubunifu wa mijadala ya umma; kufanya utafiti yakinifu, uchambuzi wa sera na utetezi na kushirikiana na wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya jarida hili kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chazo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala mbili kwa HakiElimu.

Mhariri Mkuu:
Rakesh Rajani

Timu ya SautiElimu
Godfrey Telli
Robert Mihayo
Newton Kyando na
Maria Kalavo

Picha Kwa Hisani ya:
Panos
Mpoki Bukuku
Marko Tibasima

Tuandikie!

HakiElimu SautiElimu
S.L.P. 79401
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: (022) 2151852 au 3
Faksi: (022) 2152449
Baruapepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

ISSN 1821 5072

© HakiElimu 2006

Ukurasa wa 2